# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI TUNDUMA TC

THE HEAD MASTER
TUNDUMA TC SEC. SCHOOL
P.O. Box.......
TUNDUMA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za simu**

**Mkuu wa Shule 0763590186**

**Makamu Mkuu wa Shule 0715252172**

**Matron/Patron 0757200540**

**Shule ya Sekondari TUNDUMA TC.**

**S.L.P 197**
**Tarehe…………………………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**………………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………….**
**………………………………………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI TUNDUMA TC HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA MKOA WA SONGWE MWAKA ……………...**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka……………na atasoma tahasusi ya **........... (HGK, HKL, HGE, HGL,HGLi)** (*Kata tahasusi ambayo hujachaguliwa*)

Shule ya Sekondari **TUNDUMA TC** ipo umbali wa Kilometa kumi **(10km)-kutoka kituo cha mabasi MPEMBA kwa wale wanaotokea barabara kuu ya MBEYA -TUNDUMA**. Usafiri wa daladala kutoka MPEMBA **stendi**

unapatikana katika kituo cha Mabasi **Mpemba**.Nauli ni Shilingi **700** kwa **daladala , pikipiki 3000,** na Shilingi **1000** kwa bajaji hadi shuleni.Kwa wale wanaotokea barabara kuu ya **SUMBAWANGA-TUNDUMA** washukie kituo kidogo cha mabasi **Kilimanjaro au Sogea** kutokea hapo ni umbali wa kilomita moja kufika shuleni.

Muhula wa Masomo utaanza tarehe itakayotangazwa na Serikali.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni suruali 2, **rangi ya zabibu 1**, na rangi **ya dark grey 1**).
ii. Mashati mawili (2) rangi ya light blue ya mikono mirefu
iii. Sare ya Michezo ni bukta mbili za mazoezi rangi ya bluu, raba za michezo ama viatu njumu jozi mbili
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta jeusi
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) **suruali moja rangi ya dark blue**
ix. Tai mbili zinazo endana na rangi ya suruali husika
x. Tisheti rangi ya kijivu mbili zenye kola, pia kwa watakao shindwa kupata maeneo mengine zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs.15,000/= kwa T shirt moja.
xi. Trucksuit moja rangi ya dark blue yenye ufito wa bendera ya taifa, Pia kwa watakaopenda zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs.25,000/= kwa trucksuit moja.

**NB:*Sare za shule unashauriwa kushonea shuleni ili kuepuka kukosea rangi halisi ya kitambaa na aina ya mshono***

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -**

i. Madaftari 12 aina ya counter book **quire 4**
ii. **Ream (A4)** Mbili (2) kwa mwaka kwa combination za **HGL**, **HKL** na **HGK** na **Ream A3** bunda moja (01) kwa mwaka kwa combination ya **HGE**.
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (***rejea orodha ya vitabu iliyoambatanishwa mwishoni mwa fomu hii***)
iv. Scientific Calculator; kwa wanaosoma Geography, Economics na Basic
v. Applied Mathethematics (BAM)
vi. Godoro futi mbili na nusu, na chandarua rangi ya blue Bahari

vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya blue bahari, blanket 1, foronya ya godoro 1. vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula aje na chombo aina ya kontena yenye vyumba vitatu(colabo), kijiko na kikombe.
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. Kwanja 1, jembe 1, kwa wanafunzi wa tahasusi za **HGK, HGL, HKL** na reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje kwa wanafunzi wa tahasusi ya **HGE**
xi. Folder file 1, picha 2 passport size akiwa amevaa shati nyeupe (backgroun ya blue)
xii. Nakala za vyeti vya kitaaluma (result slips na leaving certificate)
xiii. Nakala moja ya cheti cha kuzaliwa

**2.1 Michango mbalimbali inayotakiwa**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB: Michango ya uendeshaji wa shule iwekwe kwenye akaunti ya shule Na.0150659548000 jina la akaunti TUNDUMA TC SECONDARY SCHOOL BENKI YA CRDB TAWI LA TUNDUMA.**

**2.2.** Mwanafunzi aje na bima ya afya kwa ajili ya matibabu na kama hana bima ya afya aje na **Tshs.50,400/=** kwa ajili ya kukata bima ya afya kwenye mfuko wa **NHIF**, ***fedha hii isiingizwe kwenye akaunti ya shule*** ila itatolewa **control number** maalum kwa ajili ya kulipia **baada ya mwanafunzi kuripoti** shuleni

**Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha,inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu
vi. yeyote yule;
vii. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
viii. Kufuga ndevu;
ix. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
x. Uvutaji wa sigara;
xi. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja au kuoa xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale
xiii. yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**6.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB: -Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni**

**mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0763590186**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0715252172**
- **Mwandamizi Taaluma: 0683974955**
- **Mwandamizi Malezi: 0758392012**

**-Kila mwanafunzi akumbuke kuja na bima ya afya kwa ajili ya matibabu na kwa wale ambao hawana bima za afya wafanye utaratibu wa kukata.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**MUSSA HALISON MTAKATI**
**MKUU WA SHULE**

THE HEAD MASTER
TUNDUMA TC SEC.SCHOOL
P.O. Box.......
TUNDUMA

**FOMU YA KUKUBALI MASHARTI YA SHULE (FOMU HII IRUDISHWE SHULENI)**

**SEHEMU YA MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………………………………………… kidato cha ………………………….. ninakubali kujiunga na shule ya sekondari TUNDUMA TC, nikiwa mwanafunzi wa bweni. Ninakubali masharti yote na nina ahidi kufuata sheria zote za shule. Niko tayari uongozi wa shule kuchukua hatua za kinidhamu ikiwa na pamoja na kunirudisha kwa mzazi/ mlezi endapo nitakiuka masharti ya shule.

Sahihi ya mwanafunzi ……………………………………………………………………….. tarehe……………………………………….

**SEHEMU YA MZAZI**

Mimi ………………………………………………………………………………………………… ninakubali mtoto wangu kujiunga na shule ya TUNDUMA TC kuanzia tarehe……………………………………………………….Akiwa mwanafunzi wa bweni. Ninakubali masharti yote yaliyomo katika maelezo ya kujiunga na shule ikiwa na pamoja na kulipa Michango yote ya shule na kutimiza mahitaji mengine ya shule. Nitakuwa tayari kumpokea mtoto wangu wakati wowote endapo atakiuka masharti yaliyomo au kubainika kuwa ana afya isiyo ridhisha ambayo inahitaji ukaribu na matunzo ya mzazi/ mlezi mwenywe

a) Anwani yangu ya kudumu ………………………………………………………………………………….. namba ya simu ni……………………………………
b) Jina na anuani ya mzazi/mlezi wa karibu Tunduma ambaye shule inaweza kuwasiliana naye katika matatizo mbalimbali ya mtoto (kama yupo)

1. ……………………………………………........ sahihi……………………….. tarehe ………………………….
2. ……………………………………………........ sahihi……………………….. tarehe ………………………….
3. ……………………………………………........ sahihi……………………….. tarehe ………………………….
4. ……………………………………………........ sahihi……………………….. tarehe ………………………….

| Picha ya mzazi/mlezi 1 | Picha ya mzazi/mlezi 2 | Picha ya mzazi/mlezi 3 | Picha ya mzazi/mlezi 4 |
|---|---|---|---|
| | | | |

**TUNDUMA TC SEKONDARI**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI**

1. Jina kamili ……………………………………………………………………………………………………….
2. Mahali ulipo zaliwa …………………………………………………………………………………………….
3. Tarehe ya kuzaliwa …………………………………………………………………………………………….
4. Uraia ……………………………………………………………………………………………………………
5. Anuani ya nyumbani …………………………………………………………………………………………….
6. Anuani ya mzazi (kama tofauti na hiyo hapo juu) ……………………………………………………….
7. Jina la mzazi /Mlezi ……………………………………………………………………………………………
8. Kazi ya mzazi/ Mlezi …………………………………………………………………………………………….
9. Dini ……………………………………………………………………………………………………………….
10. Kidato ulichopokelewa ………………………………………….
11. Shule uliyotoka……………………………………………………………………………………………………..
12. Shughuli unazozipendelea mbali na masomo kama mpira wa miguu, mpira wa mikono, riadha, kuimba n.k ……………………………………………………………………………………………………………
13. Wilaya unayotoka ……………………………………………………………………………………………………..
14. Mtaa /kijiji……………………………………………………………………………………………………………….
15. Kata ……………………………………………………………………………………………………………………
16. Sahihi ya mwanafunzi……………………………………………………………………………………………
17. Tarehe ……………………………………………………………………………………………………………..
18. Ndugu wa karibu anuani yake, <u>mfano</u>

| S/N | JINA | UHUSIANO | ANUANI | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| | NAHUM MALAKALINGA | Baba | S.L.P 13 TUNDUMA | 0715252172 |
| 01 | | | | |
| 02 | | | | |
| 03 | | | | |
| 04 | | | | |

***NB: Ndugu walioandikwa ndio wanapaswa kushughulikia masuala ya nidhamu, maendeleo na uhamisho wa mwanafunzi husika***

- ❖ Tafadhari soma kwa makini maelezo/ Maagizo haya/ na kuyaelekeza kikamilifu ili kuepuka usumbufu usio wa walazima.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**MUSSA HALISON MTAKATI**
**MKUU WA SHULE**

THE HEAD MASTER
TUNDUMA TC SEC.SCHOOL
P.O. Box……
TUNDUMA

**TUNDUMA OWN COUNCIL**
**TUNDUMA TC SECONDARY SCHOOL, P.O.BOX 197 TUNDUMA**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR THE STUDENT (TO BE FILLED IN THE GOVERNMENT HOSPTAL ONLY)**

1. STUDENT'S NAME ……………………………………………………………………………….
2. Please examine the above-mentioned student to his fitness for joining advanced level studies following tests.
   a) Blood examination Hemoglobin ……………………………………………………………….
   b) Stool examination ……………………………………………………………………………
   c) Bilharziasis ……………………………………………………………………………………….
   d) Urinalysis……………………………………………………………………………………….
   e) Tuberculosis (TB) ……………………………………………………………………………
   f) Eye ……………………………………………………………………………………………….
   g) Abdomen ……………………………………………………………………………………….
   h) Asthma …………………………………………………………………………………………
   i) Headache ………………………………………………………………………………………
   j) Inability to eat some type of food ……………………………………………………………
   k) Skin disease ……………………………………………………………………………………..
   l) Any abnormalities noted above……………………………………………………………….
   m) Any clinic complains …………………………………………………………………………
   n) Any treatment given or recommended ……………………………………………………….
   o) Any **STD** Detected ……………………………………………………………………...

**NOTE:** In case of unhearthly deteted. It is recommended that a student should get treatment before coming to school

I have examined the student above and consider that HE is physically fit joining Advanced leve studies.

Signature of examiner ……………………………………………………….
Designation ……………………………………………………………………
Station ……………………………………………………………………….
Rubber stamp ………………………………………………………………….
Date ……………………………………………………………………….

SHULE YA SEKONDARI TUNDUMA TC MAHITAJI YA VITABU VYA KIDATO CHA V-
Mwaka ………………………

Tunashauri baadhi ya vitabu vifuatavyo vinunuliwe kulingana na masomo atakayosoma mwanafunzi na vitabu hivi ni mali ya mwanafunzi

1. **HISTORY:**
   i. Adu Boherin, (ed) General History of Africa VII Africa under colonial domination 1880-1953
   ii. David Wrouh: Modern world History
   iii. Carton J.H Hayes contemporary Europe since 1870-1958
   iv. Denis Richard: An illustrated history of modern Europe 1789-1984 7th edition (1985)
   v. Walter Dodney: How Europe underdeveloped Africa
   vi. L.E. Snellgrove: Aficans; the History of continent low price edition (1999)
   vii. Michael Tiddy: general History of Africa
   viii. Kelvin shillington: History of Africa

2. **ENGLISH IN LITERATURE**
   - **NOVELS**
     i. The Beautiful Ones Are Not Yet Born
     ii. A Man Of The People
     iii. His Excellency the head of the state
     iv. A season of Waiting
     v. Encounter From Africa
     vi. Black Mamba
     vii. Communication skills
   - **POEMS**
     i. A wounserful surgeon
     ii. Selected poems
   - **PLAYS**
     i. Betrayal In The City
     ii. I will Mary When I Want
     iii. an Enemy Of T he People
     iv. Divine Province
     v. The Bride
3. ENGLISH STRUCTURE
   i. An introduction to language –Masija Sj
   ii. Advanced level English, Practice Approach New Syllabus Nicodemus Asheli
   iii. Grammar and composition Handbook Gleoncoe Mc Growthl
   iv. Speech communication Yuredition William Brooks/Robert W. Leath
   v. Communication skills theory and practice (Michael kadeghe)
4. GEOGRAPHY
   i. General Geography by R.B. bunnet
   ii. Practice Geography for Africa by Pritchard John M
   iii. Regional Focal studies for Advance by Masabila D.T
   iv. Map reading by Mc Master
   v. Physical Geography by Msabila D.T
   vi. Geography an inert grated approach by David Waugh
   vii. Graph paper bunda 1

**5. ECONOMICS**

i. An introduction to modern economics 4th edition by phills herdwilk Khan and john Long mead
ii. Introduction to economics by Gupta
iii. Textbook of economics by Ashag Hussein
iv. Economics for advanced level paper one and two professional studies by Ambilikile

**6. KISWAHILI**

i. Jitayarishe kwa fasihi ya Kiswahili, kidato cha V na VI
ii. Mwongozo wa kujibu maswali vitabu teule V& VII
iii. Kamusi ya Kiswahili Sanifu
iv. Vuta N'kuvute by Shafi (Riwaya)
v. Kimbunga by Hajili G. Hafi (Ushairi)

PICHA ZA SARE ZA SHULE



***Suruali Dark grey na tai shati mikono mirefu rangi ya white blue***



***Suruali rangi ya zabibu na tai shati mikono***



*T-shirt rangi ya kijivu yenye nembo ya shule ya Tunduma TC Secondari*



*Track rangi ya dark blue yenye ufito wa bendera ya taifa*

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**MUSSA HALISON MTAKATI**
**MKUU WA SHULE**

THE HEAD MASTER
TUNDUMA TC SEC.SCHOOL
P.O. Box
TUNDUMA